**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: "UTUMISHI", DSM.
Simu: 2118531-4

Fax: 2125299
Barua Pepe: permsec@estabs.go.tz

Menejimenti ya Utumishi wa Umma,
UTUMISHI HOUSE,
8 Barabara ya Kivukoni
S. L. P. 2483,
**11404, DARA ES SALAAM**

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. CAC 56/507/01/14 15 Septemba, 2014

# WARAKA WA UTUMISHI NA. 2 WA MWAKA 2014 KUHUSU KUDHIBITI VIRUSI VYA UKIMWI, UKIMWI NA MAGONJWA SUGU YASIYOAMBUKIZWA MAHALI PA KAZI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Serikali katika jitihada za kudhibiti maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI (VVU) na UKIMWI, ilitoa Waraka wa Watumishi wa Umma Na. 2 wa mwaka 2006, ulioelekeza kutolewa huduma kwa Watumishi wa Umma wanaoishi na VVU na wenye UKIMWI. Madhumuni ya Waraka huo ilikuwa ni kuweka utaratibu wa namna ya kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na VVU na kuhamasisha watumishi kupima na kujua hali ya afya zao. Aidha, mwaka 2007, Serikali ilitoa Mwongozo wa Kudhibiti UKIMWI katika Utumishi wa Umma wa mwaka 2007. Mwongozo huo ulilenga kupunguza maambukizi ya VVU miongoni mwa Watumishi wa Umma na kutoa utaratibu wa kuwahudumia watumishi wanaoishi na VVU na wale wenye UKIMWI mahali pa kazi katika Utumishi wa Umma.

1.2 Kufuatia utekelezaji wa nyaraka hizi, Serikali ilifanya Tathmini kuona kama jitihada hizo zilileta matokeo yaliyokusudiwa.Tathmini hiyo iliyofanyika mwaka 2013, ililenga kubaini mafanikio na changamoto za utekelezaji ili kuboresha jitihada za kudhibiti maambukizi ya VVU na UKIMWI katika Utumishi wa Umma. Matokeo ya tathmini hiyo yalionyesha kuwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na waajiri kutoa huduma za lishe kwa watumishi wanaoishi na VVU; kupungua kwa ubaguzi, unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI. Hali hii imewezesha watumishi wanaoishi na VVU kuendelea na majukumu yao kama kawaida kutokana na afya zao kuimarika.

1.3 Pamoja na tathmini hiyo kuonesha mafanikio ya kupungua kwa maambukizi ya VVU na UKIMWI, pia ilionyesha kuibuka changamoto nyingine ya kuwepo kwa Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa (MSY). Kwa mujibu wa taarifa hiyo, zaidi ya asilimia 60 ya Watumishi wa Umma walikuwa kwenye hatari ya kupata MSY kutokana na mitindo ya maisha isiyofaa. Matokeo kama haya, yameoneshwa pia kwenye taarifa ya Utafiti wa MSY iliyofanywa na Shirika la Afya Duniani kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mwaka 2012.

1.4 Taarifa ya Utafiti huo ulionesha kuwa asilimia 27 ya Watanzania wakiwemo Watumishi wa Umma walikuwa na tatizo la Shinikizo Kubwa la Damu; na asilimia 9 walikuwa na tatizo la kisukari. Aidha, kwa mujibu wa Taarifa ya Utafiti wa Viashiria vya UKIMWI na Malaria iliyofanyika mwaka 2011/12 kwa lengo la kupata taarifa sahihi za maambukizi ya VVU nchini; kiwango cha maambukizo ya Virusi Vya UKIMWI (VVU) kitaifa kilikuwa kimefikia asilimia 5.1. Tafiti hizi zinaonesha kuwa ni muhimu kuendelea na jitihada za kuzuia VVU, na pia kupunguza kasi ya kuenea kwa MSY.

1.5 Kutokana na hali hii Serikali imeandaa "***Mwongozo wa Kudhibiti VVU, UKIMWI, na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma wa Mwaka 2014***" ambao unatoa utaratibu bora wa kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi katika Utumishi wa Umma.

## 2.0 MADHUMUNI YA WARAKA HUU

Madhumuni ya Waraka huu ni kuwaarifu watumishi wa umma kuhusu umuhimu wa kuchukuwa tahadhari kutokana na kuwepo MSY, na kuwaelekeza Watendaji Wakuu wa Wizara, Taasisi za Umma, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuutekeleza ipasavyo "**Mwongozo wa Kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi katika Utumishi wa Umma wa mwaka 2014**".

## 3.0 HATUA ZA KUDHIBITI VVU, UKIMWI NA MSY

3.1 Juhudi za kudhibiti VVU na UKIMWI na MSY katika Utumishi wa Umma hazina budi kusimamiwa kwa pamoja baina ya Mamlaka za Ajira na watumishi wenyewe kwa nafasi zao. Katika kutekeleza mwongozo huu Mamlaka za Ajira zinaelekezwa kutekeleza yafuatayo:-

3.1.1 Kuandaa na kutoa mafunzo mbalimbali yanayolenga kuimarisha afya na ustawi wa watumishi wote kuhusu udhibiti wa VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi.

3.1.2 Kuwezesha utoaji wa mafunzo maalum ya unasihi kwa Maafisa Rasilimaliwatu, Waratibu wa VVU, UKIMWI na MSY na waelimisha rika mahali pa kazi.

3.1.3 Kuwezesha upatikanaji wa huduma sahihi ya unasihi kwa watumishi wote, na kuhakikisha kuwa watumishi waliojiweka wazi kuwa wanaishi na VVU, UKIMWI na MSY wanapata huduma ya unasihi mara kwa mara kwa lengo la kuwaimarisha kisaikolojia, kiafya na ustawi wao.

3.1.4 Kuwahudumia watumishi wanaoishi na VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi wakati wote kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Kanuni za Serikali.

3.1.5 Kuchangia fedha za huduma mbalimbali kwa watumishi wanaoishi na VVU, UKIMWI kwa kiwango kisichopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) na kisichozidi shilingi laki moja (100,000/=) kwa mwezi.

3.2 Kuhusu hatua za kuchukuliwa kudhibiti MSY, Mamlaka za Ajira zinaelekezwa kuweka mazingira yatakayowawezesha watumishi kuboresha afya na ustawi wao kwa kufanya yafuatayo:-

3.2.1 Kuweka vifaa kinga na vitendea kazi kwa ajili ya kuwawezesha watumishi kukabiliana na MSY kama vile mashine za kupima shinikizo la damu, sukari, mizani za kupima uzito, na visanduku vya huduma ya kwanza,

3.2.2 Kutenga sehemu kwa ajili ya upimaji wa afya za watumishi,

3.2.3 Kutenga sehemu ya kufanyia mazoezi na kuweka vifaa vya mazoezi, na

3.2.4 Kuhamasisha ulaji bora kwa watumishi.

3.3 Kwa upande wa watumishi wa umma, wanasisitizwa kutambua kwamba mbali ya kuwa suala la afya dhaifu huathiri uwezo wao wa kufanya kazi kwa ufanisi, pia linawaathiri wao binafsi. Hivyo watumishi wenyewe wanawajibika pia kujali afya zao kama

ilivyofafanuliwa katika Kanuni 105 (2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma (Public Service Regulations) za Mwaka 2003. Hivyo kila mtumishi wa umma anawajibika kuchukua tahadhari dhidi ya vichocheo vinavyoweza kuathiri afya yake ikiwemo VVU, UKIMWI na MSY.

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO HUU

4.1 Kutokana na uamuzi huu wa Serikali, Mamlaka za Ajira zinaelekezwa kuwasilisha taarifa ya kila mwaka kuhusu utekelezaji wa "**Mwongozo wa Kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY mahali pa kazi katika Utumishi wa Umma wa Mwaka 2014**" kwa Katibu Mkuu (**UTUMISHI**).

4.2 Pamoja na kuandaa na kuwasilisha Taarifa, inategemewa kuwa Watendaji Wakuu wote wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma, watazingatia na kuyasimamia maelekezo ya Waraka huu kwa ukamilifu, ikiwa ni pamoja na kutenga bajeti katika mipango ya kila mwaka .

## 5.0 MWISHO

Waraka huu unaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2014 na unafuta Waraka wa Utumishi Na.2 wa Mwaka 2006 Kuhusu Huduma kwa Watumishi wa Umma wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI".

George D. Yambesi
<u>KATIBU MKUU (UTUMISHI)</u>